



TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA  
Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere - Kilimani  
S.L.P 1049, DODOMA  
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222  
Faksi: +255 22 2111281  
Barua Pepe: [info@chragg.go.tz](mailto:info@chragg.go.tz)  
Tovuti: [www.chragg.go.tz](http://www.chragg.go.tz)

Desemba 16, 2019

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### **Pongezi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Magufuli kwa uamuzi wake wa kutoa msamaha kwa wafungwa zaidi ya 5000.**

Itakumbukwa kuwa Desemba, 9, 2019 katika Sherehe za Maadhimisho ya Miaka 58 ya Uhuru, Mheshimiwa Rais John Magufuli alitangaza msamaha na kuwaachia huru wafungwa 5,533.

Uamuzi huo wa Rais wa kuwasamehe wafungwa aliutoa wakati akihutubia wananchi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza umekuwa ukitekelezwa na wakuu wa nchi tangu tupate uhuru mwaka 1961. Hata hivyo, uamuzi wa Rais kuwasamehe wafungwa 5533 ni wa kipekee tangu Tanzania ipate uhuru kutokana na idadi kubwa ya wafungwa aliowasehe.

Kufuatia uamuzi huo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake huo uliojaa upendo kwa wananchi anaowaongoza.

Tume inachukulia uamuzi huo wa Rais kama jambo ambalo linaweka nguvu na mkazo katika sehemu ya majukumu yake ya kuhakikisha haki za binadamu zinafurahiwa na watu wote ikiwemo wale walio magerezani.

Aidha, Tume imefurahishwa na kauli aliyotoa Mhe. Rais katika maadhimisho hayo kuhusu kusikitishwa kwake na hali ya magereza, kwani kauli hiyo inaonesha dhamira ya dhiti aliyonayo yeye binafsi na serikali yake katika kulinda na kuhifadhi haki za Wafungwa na Mahabusu katika magereza hapa nchini.

Moja ya Jukumu la Tume kwa mujibu wa ibara 130 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 6 (1) cha sheria ya Tume ni kutembelea magereza ili kuangalia uhifadhi wa haki za binadamu katika sehemu hizo na kutoa mapendekezo yanayofaa katika kuimarisha na kuboresha mazingira ya magereza yetu.

Tume imekuwa ikifanya ziara za mara kwa mara katika Magereza mbali mbali kwa lengo la kutekeleza jukumu hilo. Katika ziara zake Tume imekuwa ikigundua changamoto kadhaa zinazowakabili wafungwa na mahabusu zikiwemo mlundikano wa wafungwa na mahabusu, na kesi zao kuchukua muda mrefu kumalizika. Tume imekuwa ikitoa mapendekezo kwa taasisi husika kurekebisha hali hiyo.

